# MAIR

## Ripoti ya Mwaka ya Utekelezaji MKUKUTA - 2006/2007

# Muhtasari wa Masuala Muhimu na Hatua za Kuchukua

Hatua zinazopendekezwa na MAIR zinalenga katika mchakato. Wito wa MAIR ni juu ya kuwepo kwa mawasiliano bora zaidi yatakayowezesha kuwepo kwa uratibu ulio mzuri zaidi. Hali hii itahalalisha na kuhimiza ongezeko la raslimali kwa ajili ya mkakati wa MKUKUTA.

**Mawasiliano bora zaidi** yanahusisha kuboreshwa kwa mfumo wa kubadilishana taarifa na kuwepo kwa mijadala miongoni na baina ya wadau. Pia inamaanisha kuwepo kwa ushiriki bora zaidi wa asasi zisizo za serikali katika hatua mbali mbali za mchakato wa maendeleo.

**Uratibu mzuri zaidi wa kazi** utafuatia kuwepo mawasiliano mazuri zaidi. Kazi iliyo mbele ni kuhakikisha kuwa wadau wote wanafanya kazi kwa kulingana na muundo wa MKUKUTA wa utekelezaji na bajeti, mipango, ufuatiliaji na utoaji wa taarifa. Mchakato huu utatekelezwa na makundi madhubuti ya kila nguzo ya MKUKUTA na yale yatayojumuisha wadau kutoka nguzo zote tatu katika ngazi mbalimbali nchini. Hali kadhalika, mifumo mbali mbali ya takwimu za kompyuta itasaidia kuwezesha mchakato huu. Kazi muhimu ya usimamizi itafanywa na Kamati maalumu ya Mipango, Bajeti, na Utoaji Taarifa inayoundwa na wajumbe kutoka Wizara mbali mbali.

**Kuongeza raslimali kwa ajili ya MKUKUTA** kutahalalishwa na kuhimizwa na kuwepo kwa uratibu na upatanifu mzuri zaidi wa utendaji kazi. Michango zaidi ya Wabia wa Maendeleo itaweza kushabihiana na taratibu za sasa za bajeti ya serikali.Ushiriki zaidi wa sekta binafsi utapaswa kuhimizwa zaidi (hususan kupitia Ubia baina ya Sekta ya Umma na ya Binafsi)

## Nguzo ya Kwanza: Ukuzaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini

- **Miundombinu** ya kiuchumi inaweza kuwa kigezo muhimu zaidi katika kuchochea ukuaji wa uchumi. Inapunguza gharama za uzalishaji, hususan kwa wazalishaji wadogo na wa kati na wasindikaji wa bidhaa za kilimo. Katika kuongeza misaada, miundombinu inachukua nafasi kubwa zaidi.

- Kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza uzalisha katika **kilimo** na kukuza zaidi **usindikaji wa mazao ya kilimo**. Hili linatuhusisha kupunguza au kuondoa vikwazo kama vile upatikanaji hafifu wa huduma za mikopo na fedha.

- Tatizo la uhaba wa **nishati** lililoikumba taifa miaka ya karibuni limethibitisha umuhimu wa nishati kwa maendeleo. Ni muhimu kutafiti na kubaini vyanzo mbadala vya nishati – sambamba na lengo la sita la MKUKUTA.

- Juhudi za kuboresha Mtandao wa **barabara za vijijini** hazitii moyo sana. Juhudi za kuongeza raslimali na utekelezaji hazina budi kuwa sehemu ya mchakato wa mjadala wa sekta wa kila mwaka.

- **Mishtuko na majanga** kama ukame na kupanda kwa bei ya mafuta ulimwenguni hivi karibuni yamethibitisha kuwa uchumi bado uko katika hali tete. Mbadala wa vyanzo vya nishati, na mazao ya kuuza nje na akiba ya kutosha ya chakula ni masuala muhimu katika kuimarisha uchumi ili uweze kuhimili vishindo hivyo.

## Nguzo ya Pili: Uboreshaji wa Maisha na Ustawi wa Jamii

- **VVU na UKIMWI** umerudisha nyuma mafanikio chanya kwenye viashiria vinavyohusiana na sekta ya afya kama vile kupungua kwa vifo vya kina mama wazazi. Pamoja na juhudi kubwa iliyofanywa bado vifo hivi vimeongezeka kutoka 529 hadi 578 kwa kila vizazi hai 1000. hii ni changamoto ambayo haiwezi kupuuzwa. Ili kuikabili changamoto hii, hatuna budi kuongeza juhudi na kubuni mikakati mipya.

- **Mahusiano yasiyofaa** baina ya marika yanaleta changamoto. Kuna haja ya kuongeza hatua zinazochukuliwa kuwalinda na kuwatunza watu na makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi.

- **Makazi holela,** hususan maeneo ya mijini yamekuwa ni tishio kwa mazingira. Hali hii inaibua haja ya kubuni hatua za haraka za kulikabili tatizo hili ikiwa ni pamoja na kuyaboresha na kuyahalalisha makazi hayo yasiyopangwa.

- Kumekuwepo na ongezeko la mzigo wa **wazee** na **watoto yatima** sambamba na watoto kutoka katika **familia fukara zaidi**. Makundi haya yanahitaji namna Fulani ya hifadhi ya kijamii. Mahitaji ya fedha kwa makundi haya ni makubwa kwa hiyo ipo haja ya kubainisha walengwa. Tafiti zinahitajika ili kusaidia kufahamu uwezo na ufanisi wa hatua za hifadhi ya kijamii.

- Maendeleo ya baadaye yanategemea kuwepo kwa watu walioelimika vizuri katika fani mbali mbali hususan afya na elimu.

- Changamoto kubwa hapa ni ugharamiaji wa maendeleo ya raslimali watu inayohitajika ili kuboresha huduma za jamii. Hili si tu kwamba linalazimisha kuwepo kwa mfumo endelevu wa ulipaji wa kodi, bali pia linaleta msukumo wa madai ya kuongezeka kwa mishahara ya watumishi wa umma.

## Nguzo ya tatu: Utawala Bora na Uwajibikaji

- Uwezo mdogo wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutenga mafungu, kusimamia na kukagua raslimali, unalazimu kuwepo kwa hatua zaidi za kuimarisha uwezo wake.

- Ukaguzi wa mahesabu chini ya serikali za mitaa unahitaji kujengewa uwezo na kuimarishwa zaidi. Hitaji hili linazidi kuwa muhimu zaidi kufuatia hatua za hivi karibuni za upelekaji wa madaraka, majukumu na raslimali kwa wananchi.

- Uwekaji wa taarifa kwenye mbao za matangazo unaofanywa na serikali za mitaa katika ngazi mbali mbali hautuhakikishii kwamba umepelekea kuboreka kwa taarifa hizo kutumika miongoni mwa jamii.

## Ufuatiliaji wa MKUKUTA

- Kuna haja ya kuboresha mfumo wa taarifa za utendaji kwenye Wizara, Idara na Wakala wa serikali pamoja na,

- Wadau wote wanapaswa kufanya juhudi za maksudi kubuni mfumo ulioratibiwa vizuri wa ukusanyaji, uchambuzi na utumiaji wa taarifa.

## Ugharamiaji wa MKUKUTA

- Kuna umuhimu wa kuoanisha mipango mikakati ya Wizara, Idara na Wakala wa serikali na MKUKUTA ili raslimali ziweze kuelekezwa kulingana na mipango iliyowekwa.

- Raslimali za kugharamia MKUKUTA hazitoshelezi. Hii inailazimu serikali (a) Kuongeza mapato ya ndani (b) Wabia wa Maendeleo waongeze na kuoanisha utoaji wa misaada

- Kuna umuhimu wa kuwepo ufanisi katika (a) kuhusianisha raslimali na matokeo yanayotarajiwa (b) utoaji wa taarifa za matokeo. Hii inalazimu kuzidi kuboresha mfumo wa utoaji wa taarifa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**
Wizara ya Fedha na Uchumi,
S..L.P. 9111, Dar Es Salaam
Simu: +255 2111174, Fax: 21103226
Barua Pepe: mkukuta@gmail.com; Tovuti: www.povertymonitoring.go.tz